Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 11 -5
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412
Telephone +44 (0) 1604 765068
Facsimile +44 (0) 1604 463578
Email: CarlHinton@hotmail.com
Web: http:\\go.to\Carl_Hinton

9781902059112

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 32-36

Correspondence Course Lessons 32-36

Tena:

1 902059 00 - X	Matayarisho ya Ubatizo
1 902059 01 - 8	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 1-4
1 902059 02 - 6	Ukimwi
1 902059 03 - 4	Mshitaki Wenu Ibilisi
1 902059 04 - 2	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 5-8
1 902059 05 - 0	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 9-11
1 902059 06 - 9	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 12-15
1 902059 07 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 16-19
1 902059 08 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 20-23
1 902059 09 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 24-27
1 902059 10 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 28-31
1 902059 11 - 5	**Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 32-36**
1 902059 12 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 37-40
1 902059 13 - 1	Ufunuo mlango wa kwanza - Maelezo ya maneno ya mstari kwa mstari

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na 32.

NDOA ZA KIKRISTO

Kusoma: 1 Wakorintho 7

Kuoana na mapatano yanayo anza mbele ya mashahidi na kuorodheshwa na mtu wa Serikali, ambapo mwanaume na mwanamke wanakubaliana kuishi pamoja. Mpaka hapa kila mmoja ana juwa makusudi yao, no hivyo ndoa inafanya msingi ulio katika hali nzuri ya kulea watoto ambao wanaweza kujiona wapo salama kama sehemu ya mtu na mkewe.

Hiyo ni ndoa ya Kikristo, na zaidi. Ahadi zinazo fanywa mbele ya mashahidi pia zinakuwa zimefanywa mbele ya Mungu, nazo zinakuwa ni ahadi za kudumu. Mungu anachukia kuachana (Malaki 2:16)

Ushauri wa Kiroho ni mume mmoja na mke mmoja wataishi pamoja Wakati wote

Mume na mke

Mungu alimuumba mwanamke we kwanza, Eva, toka ubavu wa Adamu (Mwanzo 2:21-24). Angeweza kumuumba kutoka kwenye mavumbi ya ardhi, kama Adamu tu, bali alitaka kumfundisha Adamu, vile vile na sisi, kuwa mume na mke wana haki kuwa pamoja na waishi kana kwamba walikuwa “mwili mmoja” (mstari wa 24). Hii ndiyo siri ya ndoa ya Kikristo yenye furaha mume na mke wanao ishi kwa kusaidiana, kutiana nguvu na kufurahi pamoja, katika ufahamu wa kila siku wa uwepo wa Mungu.

Lakini sio kila mmoja yampasa aowe. Yesu Kristo alikaa peke yake, ne hivyo, kama tunavyo juwa, na mtume Paulo naye alikaa peke yake, ingawa alisema angeweza kuwa na mke kama angetaka mmoja. Ukweli ni kwamba watu wengine wameumbwa katika njia ambayo wanapenda kuishi bila kuowa, na wengine wanahitaji wa kushirikiana na msaada wa mume au mke. Paulo aliwashauri wale walio kuwa Korintho, ambao aliwaandikia katika wakati wa dhiki za waamini (1 Wakorintho 7:26), kuwa waowe tu kama kweli walihitaji kuowa. Watu wengine ni wabora kuweza kumtumikia Mungu kama wakibaki bila kuowa (mistari 32-35), wengine wanahitaji kuowa (mistari 2-9). Yote ni mambo ya mwili wa kila mtu na akili ilivyo umbwa.

Kuoana ni mpango aliotoa Mungu. Sio njia ya kufaa kumpata mtunza nyumba wa bila malipo au ya kutafuta mwanaume wa kukutunza. Kuna vipengele vya muhimu kujifunza na kujizoeza kama kuoana ni kwa kumpendeza Mungu, nasi tutafuatilia hata mwisho toka mwanaume anapo fikiria kutafuta mke, au mwanamke anapo amua angependa kuolewa. Somo lililotengwa lita shughulika na matatizo mengine katika ndoa, kwa sababu ya desturi maalum za ndoa au tabia tofauti.

35D Kazi ya ziada
Somo Zaburi 32 na useme kwanini Daudi aliiandika jinsi unavyofikiri. (2 Samweli 11 itakusaidia).

36A Mwishoni mwa ukurasa wa Somo 36, kuna orodha ya mambo ambayo waamini walio batizwa wayafanye. Ni nini kingine wafanye kwa kawaida?

36B Mambo gani mwamini aliye batizwa **asi** fanye?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASWALI KARATASI YA 9

Jaribu na ujibu maswali katika maneno yako mwenyewe, Mahali inapo semwa 'Kazi ya ziada' unaweza kujibu ukitaka, au kuacha ikiwa utaona ni magumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote mengine.

MASOMO 32-36

32/33A Ndiyo au Hapana?
- (a) Je Wakristo wote yawapasa waoe?
- (b) Mwamini aoe asiye amini?
- (c) Ikiwa tumefanya uzinzi tunaweza kusamehewa na kubatizwa?
- (d) Kama tumeamua kumuoa mtu fulani, tunaweza kuwa na tendo la ndoa nao kabla ya kuoana hakujafanyika?
- (e) Ndoa kati ya waamini idumu maisha?
- (f) Je wawili walio oana yawapasa wapate watoto?
- (g) Je Mungu anachukia kuachana?
- (h) Ikiwa mwamini ameoana na asiye mwamini, ni vema kuishi naye (au kumwacha asiye amini)?
- (i) Je talaka inaweza kuruhusiwa kati ya Wakristo?
- (j) Je mwenzi aliye fanya uzinzi aachwe?
- (k) Mwamini achukuwe mke wa pili?
- (l) Je ndoa kati ya wanao ishiriki ivunjwe kwa sababu wameacha kupendana?
- (m) Mtu yupo huru kuoa mwingine ikiwa mwenzi wake amefariki?

32/33B Mafungu haya ya maneno yanatufundisha nini?
- (a) 2 Wakorintho 6:14
- (b) Mathayo 5:31-32

Kazi ya ziada
- (c) Wakolosai 3:12-25
- (d) Waefeso 5:23-25
- (e) 1 Timotheo 2:9-15

34A Eleza baadhi ya shughuli (kazi) ambazo waamini waziepuke.

34B Kwa nini waamini wa kweli hawapigi kura wala hawajihusishi na siasa?

34C Yesu alikuwa na maana gani katika Yohana 18:36?

34D Kazi ya ziada
Orodhesha mambo baadhi katika 1 Petro 2:11-17 tunafundishwa nini.

35A Andika orodha ya mambo tuwezayo kuyaombea.

35B Ikiwa tunamuomba Mungu kwa busara, tutafanya **namna** gani? (ono Yakobo 1).

35C Kazi ya ziada
Yakobo 5:16 na 1 Yohana 5:14 tunaambiwa nini kuhusu sala?

Tendo la ndoa kabla ya kuoana

Kitu cha kwanza kufahamu ni kuwa kitendo cha ndoa ni kitu kingine alicho kiumba Mungu, lakini hataki kifanyike nje kabla ya kuoana.

Biblia inahukumu matumizi yote mabaya ya tendo la ndoa. Tendo la ndoa kabla ya kuoana na nje ya ndoa, umalaya, ufiraji na matendo ya uhayawani kwa udhahiri yote yamelaumiwa Sehemu ya kufaa tu kwa tendo la ndoa ni ndani ya walio oana. Biblia inasema:

> *"Msidanganyike; waasherati, hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabuuo samamu, wala wazinzi, wala wafiraji wa walawiti … hawataurithi ufalme wa Mungu" (1 Wakorintho 6:9,10).*

Hii haina maana kwamba kama tulikuwa wajinga mwanzo zamani; na ulukajikuta tukitenda dhambi, kwamba hatuna tumaini la kusamehewa. Mtume huendelea kwa kuwaambia Wakorintho kwamba baadhi yao walikuwa watenda dhambi (mstari 11) na kwamba sasa "wameoshwa", "wametakaswa" na "wamehesabiwa haki" katika jina la Bwana Yesu Kristo. Na kwamba katika maisha yetu ya mwanzo tulifanya mambo haya kijinga, sasa ni lazima tuyaache, kuungana kwa dhambi zetu, na kumuomba Mungu msamaha wa dhambi. kisha katika ubatizo wetu na kulitumikia jina lake Yesu, tunapewa mwanzo mpya wa maisha.

Mapenzi ndani ya ndoa ni dhawabu kutoka kwa Mungu; na imebalikiwa na muumba kati ya vitu vingine na kwamba tunaweza kupata watoto na kuishi kwenye familia ya kuangaliwa na upendo. Hakuna sheria ya Kristo katika idadi ya watoto inayowezekana kupatikana– Makanisa mengine huwatia moyo watu wake ili kupata idadi kubwa ya waumini. Wazazi wanapaswa kufikiria hali ya kifamilia ya watoto na kama kila kitu kingine katika maisha ya kifamilia, mume na mke watashauriana kufikia makubaliano kuhusu mpango wa familia yao. Na kufanya mapenzi kumetolewa kama njia ya mume na mke katika kujioneshea penzi lao kwa kile mmoja kwa mpango maalumu (1 Wakorintho 7:3-5).

Kumtafuta Mme au mke.

Pindi mfuasi katika Kristo anapoamua kuwa na ndoa, Mwanaume / mwanamke atataka kufahamu ni yupi wa kuoana naye, na Biblia inatuamuru wazi ambayo tunapasa kutii.

Muumini na amuoe muumini

Ikiwa wataishi pamoja kama wenzi Kiroho (Mtume Petro kama warithi pamoja wa neema ya Uzima" – 1 Petro 3:7) ni lazima washirikiane kwa imani iliyomoja, na kuelewa jinsi Biblia inavyofundisha kwa pamoja.* Muumini atakaeoana na asiye muumini atapata matatizo na ugumu na uhasama katika ndoa. Hamna cha kustaajabisha kama ilivyoandikwa na Mtume Paulo akisema:

"Msifungiwe nira pamoja (Ndoa) na wasioamini" (2 Wakorintho 6:14)

Kwa mtazamo wa Wajane

> *"Mke hufungwa na sheria kwa muda ambao mumewe anapokuwa hai; lakini kama mumewe amekufa, yupo huru kuolewa na yeyote amtakaye; Katika Bwana tu" (1 Wakorintho 7:39).*

Kuishi pamoja

Mume Mkristo anaye shughulika, na mke Mkristo mchaji ni mbaraka mkubwa, wote wawili pamoja na kwa wale wamwabuduo Mungu. Kwa maana kuwa – mume na kuutumia vizuri, mfano mzuri siku zote kwa maisha ya familia ni ule uliowekwa na Bwana Yesu Kristo. Alikuwa na usawa uliokuwa juu sana wa upendo na kuwajali wote aliokutana nao katika maisha. Hata hivyo, akiwaandikia Waefeso, mtume Paulo alieleza kwamba wanaume waonyeshe mwenendo mzuri katika familia sawa kama Kristo alivyo uonyesha kwa wafuasi wake.

> *"Maana mume ni kichwa cha mke, kama Kristo alivyo kichwa cha kanisa: naye ni mwokozi wa mwili … Wanaume, muwapende wake zenu, kama Kristo pia alivyo lipenda kanisa, na akajitoa kwa ajili yake" (5:23-25).*

Kuwa kichwa cha familia haina maana kuwa mume ameruhusiwa kuwa bwana mkubwa pande zote – akitegemea kila kitu kifanyike mara anapo agiza kitimizwe, na wakati wote akiwa na njia yake mwenyewe. Hayo hayakuwa matumizi ya uongozi wa Yesu juu ya wanafunzi wake– alikuwa katikati yao kama mtu atumikaye (Luka 22:27), na aliyafikiria mahitaji ya watu wengine kuwa ya muhimu zaidi kuliko yake mwenyewe. Ingawa hivyo, ina maana ya kutoa uongozi imara na wa hakika, kuweka mfano mwema, kuwa kiongozi wa maelekeo yote ya maisha ya familia, na kuzungumzia mambo katikati pamoja na jamaa wanaokuhusu wakati wowote yakiwa yapo maamuzi ya kuweza kufanya.

Zaidi ya yote, ina maana kwamba mume aongoze familia katika ibada na kufundisha, kuongoza familia katika sala na kusoma Biblia kila siku. Ilisemwa kwa Abrahamu na Mungu, "Namjua, ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, kufanya haki na hukumu" (Mwanzo 18:19). Basi, mume ajifikiri mwenyewe kama kichwa juu ya familia, anawajibika kwa maisha yao mbele za Mungu, na aione nyumbani pake hii jamaa yake kama kanisa dogo la Kikristo. Ni kweli, ikiwa hakuna waamini walio karibu, hii itakuwa ni nafasi pekee ya kumwabudu Mungu kwa kushirikiana na wengine, na ataishirikisha jamaa yake kwenye ibada hiyo ili kuwafundisha njia za Mungu, ingawa waamini walio batizwa ndiyo watakao shiriki katika mkate na divai.

35D Kazi ya ziada
Somo Zaburi 32 na useme kwanini Daudi aliiandika jinsi unavyofikiri. (2 Samweli 11 itakusaidia).

36A Mwishoni mwa ukurasa wa Somo 36, kuna orodha ya mambo ambayo waamini walio batizwa wayafanye. Ni nini kingine wafanye kwa kawaida?

36B Mambo gani mwamini aliye batizwa **asi** fanye?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASWALI KARATASI YA 9

Jaribu na ujibu maswali katika maneno yako mwenyewe, Mahali inapo semwa 'Kazi ya ziada' unaweza kujibu ukitaka, au kuacha ikiwa utaona ni magumu. Tafadhali jaribu kujibu maswali yote mengine.

MASOMO 32-36

32/33A Ndiyo au Hapana?
- (a) Je Wakristo wote yawapasa waoe?
- (b) Mwamini aoe asiye amini?
- (c) Ikiwa tumefanya uzinzi tunaweza kusamehewa na kubatizwa?
- (d) Kama tumeamua kumuoa mtu fulani, tunaweza kuwa na tendo la ndoa nao kabla ya kuoana hakujafanyika?
- (e) Ndoa kati ya waamini idumu maisha?
- (f) Je wawili walio oana yawapasa wapate watoto?
- (g) Je Mungu anachukia kuachana?
- (h) Ikiwa mwamini ameoana na asiye mwamini, ni vema kuishi naye (au kumwacha asiye amini)?
- (i) Je talaka inaweza kuruhusiwa kati ya Wakristo?
- (j) Je mwenzi aliye fanya uzinzi aachwe?
- (k) Mwamini achukuwe mke wa pili?
- (l) Je ndoa kati ya wanao ishiriki ivunjwe kwa sababu wameacha kupendana?
- (m) Mtu yupo huru kuoa mwingine ikiwa mwenzi wake amefariki?

32/33B Mafungu haya ya maneno yanatufundisha nini?
- (a) 2 Wakorintho 6:14
- (b) Mathayo 5:31-32

Kazi ya ziada
- (c) Wakolosai 3:12-25
- (d) Waefeso 5:23-25
- (e) 1 Timotheo 2:9-15

34A Eleza baadhi ya shughuli (kazi) ambazo waamini waziepuke.

34B Kwa nini waamini wa kweli hawapigi kura wala hawajihusishi na siasa?

34C Yesu alikuwa na maana gani katika Yohana 18:36?

34D Kazi ya ziada
Orodhesha mambo baadhi katika 1 Petro 2:11-17 tunafundishwa nini.

35A Andika orodha ya mambo tuwezayo kuyaombea.

35B Ikiwa tunamuomba Mungu kwa busara, tutafanya **namna** gani? (ono Yakobo 1).

35C Kazi ya ziada
Yakobo 5:16 na 1 Yohana 5:14 tunaambiwa nini kuhusu sala?

Katika nchi zingine, mfano mzuri wa maisha ya kufanya kazi umeendelea mno kiasi kwamba wanawake katika familia wanafanya kazi nzito zaidi. Ndoa ya Kikristo ni ushirika, na mume anayetaka kutunza maagizo ya Mungu atakuwa mwema na moyo wa kupenda kuishiriki katika mizigo yote ya maisha pamoja na mkewe na familia. Atataka kumpa "mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu" (1 Petro 3:7), na kumpenda sana kama ajipendavyo mwenyewe (Waefeso 5:28). Aina hii ya ushirika wa kiroho na vitendo utakuwa ni mapato yenye furaha kwa familia nzima. Kutafuta njia ya kufanya kazi pamoja na kushirikiana majukumu itakuwa ni njia bora ya kuwaonyesha majirani Ukristo ulivyo.

Mke wa Kikristo

Kwa muda tumetazama shughuli na majukumu ya mume Mkristo, lakini anaweza kufanya yote hayo tu, iwapo ana mke aliye tayari kuonyesha wajibu wake. Kunaweza kukawa hakuna wanawake wanao amini wanaoishi jirani, katika jambo lolote la kuwa mume atataka kutafuta mmoja ambaye ana nia kujifunza injili ya kweli na kuikubali njia ya wokovu iliyo fundishwa katika Biblia (kwa imani na ubatizo). Watu wengine wanao soma kozi hii tayari wamekwisha owa au kuolewa, mke au na mume wasio jifunza pamoja nao, na hicho ni kitu kingine cha kukiangalia katika somo lijalo. Lakini mume anayetaka mke awe na haja ndani ya moyo wake kutafuta mshirika wa kiroho, mtu awezaye kushiri katika mwelekeo wote wa maisha yake katika Kristo, na yayo hayo ni ya kweli kwa mwanamke Mkristo anayetaka kuolewa.

Sawa kama Eva alivyo umbwa toka kwa Adamu na kwa ajili ya Adamu, basi wake wawe wema kwa waume zao. Kuna neno la kupendeza sana la picha ya mwanamke (mke) mwema katika Mithali 31. "Mwanamke mwema", ameonyeshwa hapo ambaye mumewe anaweza kumwami ni kabisa, "ambaye atamtendea mema wala si mabaya siku zote za maisha yake" (mst. 12). Anafanya kazi yake kwa bidii na ya familia yake, ni mwenye huruma na mwenye ufahamu, na ni "mwanamke amchaye Bwana" (mstari wa 30).

Wanawake waaminifu wengi katika Maandiko wame ishi namna hii; waliwaepua na kuwasaidia waume zao, wakati huo wakiruhusu wawaongoze. Sara alikuwa mmojawapo wa imani na alimheshimu sana mumewe hata alimdhania Abrahamu kama bwana wake (1 Petro 3:1-6), naye alijinyenyekeza katika mambo yote. Lakini haitoshi kuwa nafasi ya pili katika familia na kumheshimu mume; mke pia ampende mumewe. Mtume Paulo alimfundisha Tito kuwa:

> *"Wawafundishe wanawake vijana kuwa na kiasi (busara), wawapende waume zao, wawapende watoto wao, wawe na akili, safi kutunza nyumba zao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe, ili neno la Mungu lisitukanwe" (Tito 2:4,5).*

Inaweza kuonekana kitu kigeni kuwasisitiza wake wawapende waume zao, lakini hili sio jambo ambalo wote wawili wanaweza kufaulu. Wanaishi pamoja ili kufaidiana na kuwa na watoto, lakini kwa kweli hawapendani. Wala hawawalei watoto wao vizuri. Lakini, maisha ya familia ya Kikristo inapasa yashirikishwe pamoja na Mungu. Kwa sababu hiyo, akina mama wana nafasi zao mbili katika kuonyesha upendo kwa familia yote, kuhusu upole ambao wanaweza tu kuutoa, na katika kuongoza na kufundisha watoto, hasa wanapo kuwa wadogo na katika kuwapakata. Maandiko yanasema kwamba wazazi "wawalee watoto katika njia ipasayo kwenda: naye hata iacha, hata atakapo kuwa mzee" (Mithali 22:66).

Hapa, basi ni jambo la Mungu: mume anaye amini na mke anaye ishiriki mibaraka iliyo tolewa na Mungu na kuilea familia ambayo pia inajifunza kweli ya Mungu. Katika njia hii utakuwa ni mbaraka kwa wote wanao kutana nao. Maisha yao yenye furaha katika Kristo, yanawaonyesha wengine mbaraka gani wanaufurahia, na hivi Mungu anatukuzwa kwenye njia zao zote.

Muhutasari

1. Ndoa ilipangwa na Mungu au ili anzishwa na ni njema na sawa.
2. Watu wengine wanataka kubakia bila kuoa, ni vema pia na ni sawa. Kweli, kubakia bila kuoa kutaruhusu ziada ya kumcha Mungu na kumtumikia.
3. Tendo la ndoa ni mbaraka wa Mungu lakini limeruhusiwa kati ya mtu na mkewe.
4. Tendo la ndoa nje au kabla ya kuoana ni dhambi na liachwe.
5. Kuoana kumeruhusiwa kwa wenye imani moja tu – na wawe wamebatizwa.
6. Waume wawatunze wake zao na watoto na kusimamia familia katika kila jambo, hasa kwa kumwabudu Mungu, kusoma Biblia na kusali.
7. Wake yawapasa wawatii waume zao na waiongoze familia kwenye njia za Mungu

Sura za kusoma: Waefeso 5; Mithali 31:10-31; 1 Timotheo 3; Wakolosai 3:12-25
Jifunze kwa moyo: Mathayo 19:5,6

"Kwa sababu hii mtu atamwacha babaye na mamaye, naye ataambatana na mke wake: nao hao wawili watakuwa mwili mmoja. Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Alicho kiunganisha Mungu mwanadamu asikitenganishe."

KOTI YA BIBLIA KUTOKA CHRISTADELPHIAN Na.33
MATATIZO KATIKA NDOA

Kusoma: Mathayo 19

Kusudi la Mungu katika ndoa ya Kikristo ni
Kwa waamini wawili kuishi pamoja kwa utukufu wa Mungu

… kuwapenda ndugu zetu wa kiume na wa kike:

> *"Wapendwa, tupendane: maana pendo nila Mungu; na kila apendaye amezaliwa na Mungu, na amjua Mungu" (1 Yohana 4:7).*

…kuwa hurumia watu wengine, na kuwasaidia popote tunapo weza:

> *"Basi yoyote mnayotaka mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo" (Mathayo 7:12).*

…usishiriki katika vitendo vya uasi vya ulimwengu:

> *"Tokeni kati yao, na mjitenge asema Bwana; msiguse kitu kichafu; nami nitawapokea, nitakuwa Baba kwenu, nanyi wanangu wa kiume na wakike asema Bwana Mwenyezi" (2 Wakorintho 6:17,18).*

. . juu ya yote zaidi, kumpenda Mungu kwa fahamu zetu zote:

> *"Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" (Kumbukumbu 6:5).*

Sura za kusoma: 1 Wakorintho 13; Luka 10:30-37; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-28
Mstari wa Kujifunza: 2 Wakorintho 5:17

> *"Kwa sababu hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa ni kiumbe kipya: ya kale yame kwisha pita; tazama yote yamekuwa mapya".*

Kazi ya kuwatawadha miguu ilikuwa ni kazi ya mtumwa. Hata hivyo hiyo ilifanywa na Yesu na baadaye aliwaambia "Nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyo watendea nanyi mtende" (Yohana 13:15).

Aliwatumikia wanafunzi wake kwa upendo na unyenyekevu, nasi yatupasa kutumikiana. Ndipo tutakuwa aina ya watu ambao Mungu awataka kuishi katika Ufalme wake.

"Heri wapole, maana hao watarithi nchi" (Mathayo 5:5).

Kumkumbuka Yesu

Tunashika njia, wakati tukibatizwa, njia iliyo nyooka na nyembamba inayo elekea Ufalme wa Mungu. Lakini hata sasa tunabakia kuwa wanadamu, na, kwa urahisi tunaweza kusahau ni kiasi gani alicho tufanyia
Yesu alipo kufa kwa ajili yetu.

Yesu alijua kiasi wanafunzi wake watakavyo msahau; basi aliwaambia kitu kingine cha kuwakumbusha. Fungua Injili iliyo andikwa na Luka 22:14-20. Hii ilitokea wakati wa chakula cha mwisho tulicho kizungumzia, wakati Yesu alipotawadha miguu ya wanafunzi.

Ona jinsi mkate na divai ilivyo kuwa inawakumbusha namna Yesu alivyo toa uhai wake kwa ajili yao. Aliwaambia "Fanyeni hivi kwa kunikumbuka".

Sasa soma 1 Wakorintho 11:23-28. Wakristo wa kwanza walikutana katika siku ya kwanza ya juma iii kumkumbuka Yesu kwa njia aliyo waamuru.

Wafuasi wa kweli wa Bwana Yesu watakutana pamoja, kama wanafunzi wa kwanza walivyo fanya (na mara kwa mara Jumapili ni siku iliyo faa zaidi kwa mikutano kama hii), kuumega mkate na kunywa divai, kukumbuka jinsi mwili wa Yesu ulivyo tolewa na damu yake ilivyo mwagika kwa ajili yao.

Kama tunavyo kuwa katika Kristo, kumkumbuka Yesu katika njia hii itakuwa ya muhimu zaidi na zaidi kwetu, kwa kutusaidia kuelewa kwamba yeye yu pamoja nasi wakati wote.

KUENENDA KATIKA UPYA WA UZIMA MAANA YAKE…

…kusoma Neno la Mungu kila siku:

"Kuingia kwa maneno yako kwa tia nuru; kumpa ufahamu mjinga." (Zaburi 119:130.)

…kumuomba Mungu na kumsifu Yeye siku zote:

"Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila kitu kwa kusali na kuomba na kwa - = kushukuru na haja zenu nazijukane na Mungu" (Wafilipi 4:6).

Lakini haiwezekani siku zote kulifikia kusudi hilo. Matatizo yanatokea na somo hili linayatazama baadhi, zaidi yaliyo ya kawaida. Iwapo una shida zingine, unaweza kuwasiliana na mfunzi wako ili kupata mwongozo maalum.

Kuoana na asiye amini

Waaminio waoane na wanao amini (2 Wakorintho 6:14). Lakini ni vipi kuhusu wale walio oana tayari wakati wamekuja kujuwa makusudi ya Mungu. Je, watengane, au wakae na mshirika asiye amini?

Hili lilikuwa ni tatizo la kawaida katika karne ya kwanza. Kama injili ilivyo hubiriwa, na watu walipo iamini, walibatizwa katika jina linalo okowa la Yesu. Lakini mara nyingi familia zao zilibaki katika hali ya kutoamini na kukawa na mgawanyiko ndani ya familia. Wange fanya nini: watengane na kwenda njia zao tofauti, au wakae pamoja na watatue matatizo yao?

Ushauri wa Agano Jipya unaonyesha jinsi maisha ya kuoana yalivyo machoni pa Mungu. Tunapo owa, tunakuwa na wajibu kwa wengine. Itakuwa ni ujinga kuwaacha wale tunao wapenda wakati kuna matumaini mengine ya kuifanya ndoa iendelee. Badala yake tuonyeshe imani yetu katika familia. Hivyo Biblia inatuambia kukaa pamoja kwa kadri tunavyo weza, na kwa tabia yetu kama-ya Kristo tunaweza kuionyesha kwa washirika wetu namna ulivyo upendo wa Mungu, katika Yesu Kristo:

"Ninyi wake, watiini waume zenu, kusudi ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao pasipo Neno. Wakiutazama mwenendo wenu safi (tabia njema) na wa hofu (hofu ya kumcha Mungu)." 1 Petro 3:1,2	"Na mwanamke ambaye anamume asiye amini, na kama mume huyo anakubali kukaa naye, asimuache mumewe. Maana yule mume asiye amini hutakaswa katika mkewe, na yule mke asiye amini hutakaswa katika mumewe: kama isingekuwa hivyo watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu. Lakini kama yule asiye amini akiondoka, na aondoke." 1 Wakorintho 7:13-15
Maandiko haya yanafundisha kwamba kila kitu kina cho wezekana kifanyike ili kuitunza ndoa pamoja	

Mungu ataihesabu ndoa iliyo fanywa mbele ya mshirika mmojawapo aliye uelewa ukweli wa Biblia, kama ni uhusiano mtakatifu, na watoto hawata onwa kuwa hawakubaliwi. Mwito ni kujaribu kuineza kweli ya Kristo ndani ya familia, kwa mfano wako mzuri.

Kama matatizo katika ndoa yakitokeza, yakabiliwe sawasawa, kwa kukumbuka kwamba kuna majukumu katika hali zote ili kuifanya ndoa iendelee. Hii inaweza kuwa na maana kukubali kuileta katika hali inayokusudiwa zaidi - lakini hicho ndicho Yesu alicho fanya alipo kufa ili tuweze kuwa na tumaini la wokovu.

Biblia inailinganisha ndoa na uhusiano kati ya Kristo na waamini, hivyo mfano wake utatusaidia wakati shida inapo tokea. Mara nyingi talaka imeonekana kama njia ya kutokea. Ikumbukwe kuwa kabla ya kuchukua hatua kama hii ya mwisho kwamba.

Mungu anachukia kuachana (tazama Malaki 2:16)

Kuoana kati ya waamini

Mungu ameagiza maisha ya ndoa kama uhusiano wa kudumu. Ahadi za kuoana hazifanywi kuwa zivunjwe; zinafanywa ili zitunzwe maisha yote. Wakati mshirika mmoja wa ndoa afapo, mwenzake anaye bakia yupo huru kuoana na mwingine tena (Warumi 7:2,3).

Kitu kisicho kubalika kwenye sheria yote ambayo ndoa baina ya waamini ni ya kudumu inatokea wakati mmoja wa washirika si mwaminifu katika tendo la ndoa. Mara moja Yesu aliwahi kuulizwa alifikiri nini wakati mmoja wa washirika wa tendo la ndoa anapo kuwa sio mwaminifu kwa sababu Wayahudi walizoea kuendelea kutoa talaka kirahisi (mamlaka zilitoa hati ya kuthibitisha tu, na ndoa inakuwa imefikia mwisho). Waulizaji wake walitaka kujua kama Yesu alidhani ndoa ilikoma **mbele za Mungu** katika njia hii.

Bwana Yesu aliwatajia Mwanzo 2 wasikilizaji wake - daima ndoa ya kwanza - na aliwakua mbusha yaliyo semwa: "Alicho kiunganisha Mungu pamoja", alisema, "mtu asikitenganishe" (Mathayo 19:6). Tambua kwamba Mungu ana angalia ahadi za kuoana zinazo fanywa mbele Zake kama nadhiri iliyo fungwa kwa ahadi. Aliulizwa zaidi kuhusu mapatano yalio ruhusiwa katika siku za Musa, Yesu aliongeza habari yote hii muhimu: Sasa Mungu ana ruhusu kuachana mahali ambapo ndoa inavunjika kwa tendo la ndoa nje ya kuoana:

> *"Yeyote amwachaye mke, **isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati**, naye akaoa mwingine, afanya uzinzi: naye amuoaye yeye aliye achwa afanya uzinzi" (Mstari 9).*

Kwa hiyo ndoa ya waamini wa Kristo ni ya maisha. Lakini ikiwa mmoja wao akiwa mwasherati (akifanya tendo la ndoa na mtu mwingine), ndoa inawekwa chini ya dharau kubwa. Ndoa isifikiriwe kana kwamba imekwisha: nabii Hosea alikuwa na mwanamke asiye mwamini fu, lakini alijitahidi kumvuta amrudiye mwenyewe, kwa sababu alimpenda mwanamke. Kuachana kutazamwe na wa-Kristo kama kimbilio la mwisho. Yatupasa tukumbuke kwamba tuwe tayari kusamehe mabaya ya mshirika wetu katika ndoa aliyo tutendea kama tunataka kusamehewa na Mungu wakati tunapo mkosea. Kama kwa sababu ya kutokuwa mwaminifu mwenzi mmoja, hatimaye kuna kuachana, kila tahadhari ichukuliwe ili kuzuia kufanyika madhara kwa jamaa wengine wa familia. Jamaa aliye achwa asitake kuolewa tena; siku zote kwa wawili waweze kuishi maisha ya kutengana mara ndoa ifikapo mwisho.

Jambo lililo kubwa la kuweza kuwafanyia ni kuwapitishia habari njema za Ufalme wa Mungu, ambazo sisi wenyewe tumeziamini. Kama Mungu alivyo tualika sisi kushika njaa zake na kushiriki katika furaha ya Ufalme, hivyo nasi tutataka kuwa alika wengine kuja kushiriki katika mambo haya.

Kuomba na katika kutoa ibada

Tunapobatizwa katika Kristo, tunakuwa wana wa Mungu, na tunaweza kuja kwake kwa njia ya sala, kumwabudu Yeye na kumuomba msaada wake katika maisha yetu.

Bado inatubidi kamwe tusisahau ukuu wa Mungu ulivyo. Utukufu na enzi yake vipo nje ya ufahamu wetu. Twasoma katika Isaya 57:15:

> *Maana asema yeye aliye juu, aliye tukuka akaaye milele, ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipo inuka, pamoja naye mwenye roho iliyo tubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu na kuifufua mioyo yao walio tubu."*

Yakobo anatuambia kwamba Mungu "huwapinga wajikuzao, lakini huwapa neema" (Yak.4:6). Hata Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, alijisema mwenyewe kuwa yeye ni "mpole na mnyenyekevu wa moyo" (Mathayo 11:29).

Basi wakati tunapo mjia Mungu katika sala, twahitajika. kukumbuka maneno ya mitume, ambao wanasema tumtumikie Mungu kwa kicho kinacho kubalika pamoja na hofu. Kwapo tukija kwa Mungu katika roho hii, pasipo shaka atatusikia.

Heri wapole

Katika ulimwengu huu pasipo kigeugeu tumeambiwa tupiganie haki zetu. Wale ambao wanajisimamia wenyewe wanastaajabiwa. Swali kubwa katika akili ya kila mmoja ni "Nawezaje kutoka katika maisha?"

Hii sio njia ya Mkristo. Paulo aliwaambia watakatifu waliokuwepo Philipi:

> *"Katika unyenyekevu wa moyo na kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake" (Wafilipi 2:3) Hicho ni kitu kigumu Kuweza kufanya;*

sisi sote tunapenda kujiona tu wabora kuliko mtu mwingine! Lakini tumeambiwa "Tutumikiane kwa upendo" (Wagalatia 5: 13) , na katika hili, kama katika mambo yote, Yesu ni mfano wetu. Sio muda mrefu kabla ya kifo chake, wakati aliposhiriki chakula cha mwisho na wanafunzi wake,

> *"Yesu akaweka kando mavazi yake; na akachukua kitambaa akajifunga kiunoni kisha akamimina maji katika bakuli akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu na kuifuta kwa kitambaa alicho kifunga kiunoni" (Yohana 13:4,5).*

Kuwa na haki kwa familia iliyopo ulimwenguni pote

Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mumemvaa kristo. Hapana Myahudi wa Myunani hapana mtumwa wala mtu aliye huru, hapana mwanaume wala mwanamke; maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:27-28)

Haidhuru wewe ni nani, au unaishi wapi; ikiwa umekuwa ni m-Christadelphian kwa kubatizwa katika Kristo, wote wa-Christadelphian wengine ni ndugu zako wa kiume na wa kike. (Kumbuka jina 'Christadelphian' maana yake ni 'ndugu katika Kristo'.) Ni furaha kubwa kuwa katika familia kama hii, ambayo inapatikana ulimwenguni pote.

Yesu aliwaambia wafuasi wake kabla ya kifo chake - na hata sasa anatuambia leo:

> *"Hii ni amri yangu, mpendane, kama nilivyo wapenda" (Yohana 15:12).*

Alitupenda mno sisi, hata akafa kwa ajili yetu. Akatoa uhai wake kwa ajili yetu, hivyo anasema mtume Yohana, "imetupasa kutoa uhai wetu kwa ajili ya ndugu" (1 Yohana 3:16).

Tunajua jinsi ya kuenenda mbele ya kila mmoja wetu, lakini katika matendo, ni vigumu mno. Utu wetu wa kale unachukua muda mrefu kufa! Baadhi yetu ni wepesi kukasirika; wengine wana mioyo mizito na wepesi kuchomwa; wote sisi tuna makosa yetu.

Haya ndiyo mambo tunayo takiwa kupingana nayo, kama tunajaribu kuuonyesha kwa ndugu zetu wa kiume na wa kike upendo katika Kristo upendo aliotuonyesha Yesu. Kuna picha ya upendo katika 1 Wakorintho 13. Soma mwenyewe. Hapa tuna mistari 4-7:

> *"Upendo huvumilia, hustahimili na hufadhili, upendo hauna wivu na maringo upendo haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu; bali hufurahi pamoja na kweli; huamini yote; huvumilia yote na hutumaini yote"*

Kumpenda jirani yetu

Mwana-sheria aliwahi kumjia Yesu, na alimuuliza ni amri ipi kubwa. Yesu akamwambia:

> *"Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili yako yote. Na hii ni amri kuu ya kwanza. Na ya pili ni hii nayo yafanana na ya kwanza, Umpende jirani yako kama nafsi yako" (Math.22:37-39).*

Soma habari ambayo Yesu aliisimulia katika Luka 10:30-37 inayo husu jirani mwema. Ikiwa mtu yeyote ana shida, tumsaidie. Tusiache na kufikiri iwapo tunampenda au la, au iwapo anastahili msaada wetu.

Mwanaume kuishi na wanawake zaidi ya mmoja

Wanaume wengine - hasa nchi za Kiislamu - wanaweza kuwa na mke zaidi ya mmoja wakati wanapokea injili ya Kristo. Wafanye nini - watengane na wake zao au waendelee kama walivyo?

Kuwa na mke zaidi ya mmoja, watu walizoea wakati fulani katika nyakati za Biblia. Mfalme Daudi alikuwa na wake kadhaa, mfalme Sulemani alikuwa na wake mamia na masuria. Lakini shauri la Mungu siku zote lilifahamika: Mungu alikuwa na maana ya mwanaume mmoja na mwanamke mmoja waishi pamoja kama mume na mke

Popote mipango mingine ilipo fanywa, isiende tena mara nyingi kwenye matatizo na kukosa furaha. Yesu aliiweka wazi kabisa kwamba sasa kuna njia moja tu inayo kubalika ya kuishi pamoja: "Kwa sababu hii mtu atamwacha baba na mama yake, naye ataambatana na mkewe: nao wawili watakuwa mwili mmoja" (Mathayo 19:5).

Hapana mtu anaye weza kuchukuwa mke zaidi ya mmoja kwa sababu hii baada ya kubatizwa katika Kristo. Vipi wale walio nao kadhaa tayari? Ushauri wetu ni kuwa yeyote aliye nao kadhaa hao wake zake bado awaangalie mwenyewe kama anao wajibu kwao wote, na aendelee kuwa mume mwema na baba yao wote wanao mtumaini (wanao mtegemea). Wakristo hawayaachi majukumu yao wakibatizwa, wanachukuwa tahadhari zaidi kwa ajili ya wanao mtegemea. Christadelphian Bible Mission inatoa ushauri huo kwa sababu ya ndoa za mitari hazitimizi mifano kamili ya kuitazama ya Mkristo, ndugu huyu hatakuwa "mzee" wa eklezia la Christadelphian.

Arusi ya kuoa

Matatizo yametokea yanayo husu gharama za sherehe ya kuoa wakati vijana wawili hawawezi kupata kuigharimia. Hiyo ni sababu kwanini watu katika nchi zingine wanaishi pamoja pasipo kuoana, wakikusudia kufunga ndoa wakati watakapo pata, lakini mara nyingi kamwe hawafiki hapa na pale kwenye jambo hilo. Wakati huo huo watoto wao wana zaliwa nje ya ndoa, bila usalama wote unao pashwa. Mwamini afanye nini?

Mwanaume au mwanamke waungane pamoja kama mume na mke (waoane) **kabla** ya kuishi pamoja. Tendo la ndoa kabla ya kuoana ni dhambi Biblia inasema: "Ndoa iheshimiwe na watu wote, na malazi yasi chafuliwe: waasherati na wazinzi Mungu atawahukumu" (Waebrania 13:4)

Yote yanayo hitajiwa ni sherehe rahisi ya kuoa pamoja na baadhi ya familia yetu na marafiki, na uwepo wa afisa wa kufungisha ndoa. Hapata hitajika gharama ya kuhusu chakula kinacho tolewa; ifanye wazi kwamba ufikirie jambo la muhimu zaidi kuliko kusherehekea. Wala haina tabu mahali ifanyikapo arusi.

Mahali popote pakubwa pa kutosha wale wanao hudhuria patafaa, lakini epuka kwenda kanisani kuozwa na mtu mwingine ambaye hajui mafundisho ya kweli ya Biblia. Nadhiri za ahadi ya kuoana, zinazo fanywa mbele ya mashahidi, zina maana kwamba wawili wataishi pamoja mbele za Mungu kwa maisha yao yaliyo baki. Usichanganye sherehe ya Mkristo pamoja na taratibu zingine za kuoa ambazo asili yake ni kutoka upagani: Mkristo ayaache nyuma mambo ya kipagani. Kama ikiwezekana ndoa iorodheshwe na mamlaka ya Serikali, ili kupata cheti cha ndoa.

Wakati mwingine kuna matatizo ya kulipa mahari ya juu, na itamchukuwa muda fulani kwa kijana kutunza fedha za kutosha ili kulipa mahari kwa msichana aliye mchagua. Ikiwa anaoa toka katika familia ya Kikristo, kwa kweli hawata taka kumtoza gharama kubwa, bali watamtia moyo kijana na mwenzi wake waanze kuishi pamoja pasipo shida nyingi. Lakini ikiwa bei ni kubwa, hakuna cha kufanya bali mwenye kuposa asubiri hadi ana pesa za lazima. Wakati huo huo, wote wawili wapendanao wajitunze wenyewe na kuwa safi kwa muda mpaka watakapo weza kuoana.

Kutafuta mume au mke mwema

Tatizo gumu zaidi linaelekea kuwa lile la kutafuta mume au mke mwema aliye Mkristo hasa kama kuna waamini wachache tu wanao ishi karibu. Jambo la kwanza kukumbuka ni kwamba ubora wa mambo matakatifu ya mwenzi wa baadaye ni muhimu zaidi; zaidi sana kuliko sura au utajiri. Mungu anautazama moyo, na sio upande wa nje (1 Samweli 16:7), nasi tufanye hivyo.

Wakati wowote inapo wezekana tuoane na watu Wenye imani moja, tukishirikiana katika kitu Kimoja cha kweli tunacho sadiki

Lakini kunaweza kuwa hakuna mtu, au hakuna anaye faa. Katika jambo hilo uchaguzi wa mume au mke ufanywe na bidii ya kuomba Mungu. Abrahamu aliingia katika shughuli kubwa ya taabu ya kumtafutia mke mwanawe Isaka, nasi tutahitajika kuchukuwa tahadhari ile ile na matayarisho.

Ikiwa hakuna hata mmoja ambaye tayari amekuwa ni mwamini aliye batizwa, inakupasa kufanya kile kinachowezekana ili kuweza kutafuta mume au mke mcha Mungu. Katika nchi zingine inawezekana kwa vijana kukutana kabla ya kuoana; katika jambo hilo kuna kila nafasi ya kujadili kuhusu imani za dini na kueleza mafundisho ya Biblia. Baada ya ubatizo, ndipo unaweza kuoa. Bali katika nchi ambazo mikutano hii hairuhusiwi, au kama zipo ndoa zilizo pangwa, jaribu kuchagua msichana kutoka familia inayo ishi vizuri na ujaribu kumfundisha mafunzo ya kweli ya Biblia baada ya kuwa umeoa. Lakini kabla ya kuoa, hakikisha anajiheshimu vema, anamwamini Yesu Kristo, na hakikisha unasali (au unaomba) kuhusu uamuzi utakao fanywa na kuujadili pamoja na waamini wengine kama ukiweza.

> *"Kama watoto wachanga, waliozaliwa yatamanini maziwa ya akili ya neno, iii muweze kukua"*
> *(1 Petro 2:2).*

Mungu ametupa Biblia iwe ni kitabu - cha kutuongoza. Kitatusaidia kuishi kama anavyopenda sisi tuishi, na kukua ndani ya huo 'utu mpya' katika Kristo Tunasoma katika 2 Timotheo 3:15,17;

> *"Maandiko yote yametolewa kwa maongozi ya Mungu, na yafaa kwa mafundisho na kwa kukaripia, kwa kuonya, kwa kuwaamuru katika haki, ili mtu wa Mungu akamilike, amekamilishwa vema apate kutenda kila tendo jema."*

Kuangalia mbele kwenye Ufalme

Mtume Petro anatuambia kwamba Mungu "hapendi mtu yeyote apotee" (2 Petro 3:9), na katika Yohana 3:16 tunasoma kwamba Mungu alimtuma Yesu, Mwana wake mpendwa, ili kwamba "yeyote amwaminie asipotee, bali awe na uzima wa milele".
Mungu anataka kutupa uzima wa milele katika Ufalme wake. Na sasa anatutayarisha kwa ajili ya uzima huo. Anatutaka sisi tuwepo pale, na atatusaidia katika kila njia inayo wezekana. Ametupa Yesu ili atusaidie, na kwa njia ya Yesu tunaweza kumjia katika sala.

Msaada kutoka kwa Yesu

Mara moja Yesu aliwahi kuwaambia wafuasi wake:

> *"Msiogope enyi kundi dogo; kwa maana Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi Ufalme" (Luka 12:32).*

Mara moja tena Yesu alitoa ombi la ajabu kwa Mungu kwa wale wanao mwamini. Unaweza kusoma katika Yohana 17, Angalia maneno ya mstari wa 24:

> *"Baba, hao ulio nipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulio nipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu."*

Yesu anatutaka sisi pia kuwepo katika Ufalme wake. Hivyo atatusaidiasisi katika safari na kamwe hatatuacha kufanya bidii sisi peke yetu. Yesu sio tu ni mwokozi ambaye dhambi zetu zaweza kusamehewa; pia yeye ni kiongozi katika maisha. Atashiriki maisha yetu, pamoja na mambo yote ya kwenda juu na kwenda chini na katika furaha na huzuni, na atatusaidia ili tufae kuishi pamoja naye katika Ufalme wa Mungu.

Basi mtume Petro, aliye mjua Yesu vema mno wakati alipo kuwa duniani anasema:

> *"Mumtwike fadha zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana na mambo yenu" (1 Petro 5:7):*

Muhutasari

1. Yatupasa kumkaribia Mungu katika njia aliyo amuru.
2. Mungu atasikia maombi yote ya wale walio wanyenyekevu na wanyoofu.
3. Tutoe sifa na shukrani, tukiri dhambi zetu na kuomba mwongozo wa Mungu na baraka.
4. Yatupasa kujifunza kuomba mambo yaliyo sahihi katika njia iliyo sawa.
5. Sala ni tuzo kubwa na ni baraka; inatubidi kuomba mara kwa mara.
6. Tukiisha batizwa tutaweza kuomba kwa kupitia Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya kusamehewa dhambi zetu. Wakati huo Mungu atakuwa Baba yetu na vilevile Mungu wetu.

Sura za Kusoma: Matendo 10; Zaburi 51, 102; Luka 18:1-14
Jifunze kwa moyo: Wafilipi 4:6

"Msijisumbue kwa neno lolote: bali kwa kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu nazijulikane na Mungu"

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na 36.

KUENENDA KATIKA UPYA WA UZIMA

Soma: Warumi 6

Mwanzo mpya

Tukiisha kubatizwa, tunaanza maisha mapya. "Tumezikwa pamoja naye (Kristo) kwa ubatizo katika mauti yake" wakati tukizamishwa katika maji ya ubatizo wetu. Maisha tuliyo ishi hapo awali yanakuwa yamefikia mwisho - inakuwa ni kitu kilicho pita. Kisha, kama "Kristo alivyo fufuka kwa utukufu wa Baba kutoka wafu", nasi vivyo tuenende katika upya wa uzima (Warumi 6:4).

Mabadiliko kama haya yanawezekana tu kwa neema ya Mungu. Kuwa watoto wa Baba aliye mbinguni, tunaweza kumjia kwa njia ya Yesu. Tutashindwa mara kwa mara kama tukijaribu kumpendeza Yeye, lakini wakati tukiomba msamaha, Atatusikia kwa ajili ya Kristo Yesu.

"Basi natukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati mahitaji" (Waebrania 4:16).

Kuyilisha katika Neno la Mungu

Mtoto anahitaji chakula na haja yake anaifanya ijulikane sio katika njia isiyo yakini Chakula ni cha lazima kwa makuzi. Na wale walio zaliwa katika maisha mapya kwa ubatizo wanaweza kukua katika Kristo kama maisha mapya yatashibishwa na kulishwa kwa njia ya Neno la Mungu. Hivyo mtume Petro anasema:

Sio matatizo yote ya ndoa ya Kikristo yanayo pasa kutatuliwa, ingawa somo hili limeangalia shida zingine za kawaida. Kidogo, ni baraka kubwa toka kwa Mungu - moja ya kufurahia pamoja katika maisha yote yenye furaha. Yaliyo eleweka na kuishi vema, maisha ya familia yanaweza kuwa ya juu sana; hivyo yaliyo sawa sawa ili kwamba Kuja Mara ya Pili Yesu duniani, anapokuja kuuweka Ufalme wa Mungu duniani, katika Maandiko kumelinganishwa na mwanzo wa maisha ya Mkristo aliye owa:

"Tufurahi na tushangilie, na tumpe heshima yake: maana arusi ya Mwana Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari" (Ufunuo 19:7).

Muhutasari

1. Kusudi katika ndoa ni la kudumu-maisha kati ya mume aaminiye na mke anaye amini. Kutafuta mwenzi Mkristo.
2. Ikiwa tayari tumeoa wakati tumeongoka, yatupasa kubaki na washirika wetu katika ndoa pamoja na tujaribu kuwaonyesha njia ya Mungu.
3. Nadhiri za kuoana sio za mzaa na zisicgukuliwe kirahisi. Ikiwa baada ya jitihada zote kushindwa katika ndoa zimeshindikana, basi ushauri utafutwe toka wa wazee au toka kwa mfunzi.
4. Kwa wale wanao owa mke mmoja na mume mmoja ni kusudi kamili. Kama tayari mtu ana zaidi ya mke mmoja wakati anaongoka, basi abakie kuwa mwaminifu na mume wao wote. Asichukue tena wake wengine zaidi.
5. Owa kwa haki na mbele za Mungu, hata kama unaweza kupata tu arusi rahisi.

Sura za kusoma: Mwanzo 24; Mathayo 5:31,32; Zaburi 128; 1 Timotheo 2
Jifunze kwa moyo: Waebrania 13:4

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi: lakini waasherati na wazinzi Mungu atawahukumu."

KOZI YA BIBLIA KUTOKA CHRISTADELPHIAN Na 34

WAJIBU TULIO NAO KWA SERIKALI

Kusoma: I Petro 2

Muhutasari: **Serikali ni nchi tunayo ishi, viongozi wake au utawala na sheria zake na amri**

Katika historia yote Mungu amekuwa akijitayarishia watu wake mwenyewe ambao wanafahamu madhumuni yake na watakao shiriki pamoja mibaraka ya Ufalme, na furaha ya uzima wa milele. Katika nyakati za Biblia watu hao waliishi kama taifa – taifa la Israeli ambalo Mungu alikuwa ni Mfalme wake. Wakati huo kulikuwa hakuna utata kati ya Serikali na mwamini. Sasa mambo yamebadilika, na tunahitaji kuona wajibu wa Mkristo kwa - Serikali, hasa pamoja na kuangalia mambo haya kama siasa na vita.

Watu wa Mungu

Hata sasa Mungu anatayarisha watu kutoka mataifa yote, watakao kuwa ni kitovu cha nia yake katika Ufalme. Mtume Yohana aliona maono ya jumulia hiyo, naye aneieleza kama ifuatavyo:

> *"Mkutano mkubwa, ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, wa mataifa yote, na jamaa, na watu, na lugha, ulisimama mbele ya kiti cha enzi na mbele ya Mwana kondoo, ulivikwa mavazi meupe, nao wana mitende mikononi mwao: walipaza sauti, wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye kwenye kiti cha enzi, na kwa Mwana Kondoo" (Ufunuo 7:9,10)*

Watu hao watakusanywa pamoja, atakapo rudi duniani Bwana Yesu Kristo, kutengeneza taifa jipya – taifa In Mungu mwenyewe – nao watatawala na Mfalme Yesu kwa miaka 1000 ya Ufalme duniani (angalia Ufunuo 5:9,10; 20:4)

Ufalme wa Mungu uliwahi kuwepo mara moja, zamani, wakati wafalme walipo kaa juu ya kiti cha enzi cha Mungu Yerusalemu na walitawala juu ya Israeli. Ufalme utakuwepo tena wakati Mfalme Yesu atakapo rudi (angalia Matendo 1:6; Luka 1:32,33).

Ufalme wa Mungu: katika wakati uliopita

Miaka 3,500 iliyo pita, kwenye Mlima Sinai, Mungu aliwakusanya watu wa Israeli, ambao kwa namna mpya waliokoka toka Misri, na alifanya agano (au makubaliano) pamoja nao. Walikuwa wawe taifa Lake, naye alikuwa awe Mungu wao. Walikuwa washike sheria alizo wapa kwa kupitia kwa Musa, ndipo wangeirithi nchi ya Kanaani – ambayo sasa tunaijua ki Israeli. (Soma Kutoka 19:1-8). Sheria za Mungu zilikuwa ni sheria za Serikali. Baadaye, Mungu aliwachagua wafalme kwa ajili ya watu Wake. Jeshi la mfalme lilikuwa ni jeshi la Mungu, na vita vyake vilikuwa ni vita ya Mungu. Alikuwepo mfalme kufanya kama Mungu alivyo mwamiru.

Wakati ule yote hayo yalibadilika. Wafalme walisahau sheria za Mungu, wakafuata mfano mbaya wa mataifa yaliyowazunguka na, mwishowe, Mungu aliamua kuukomesha Ufalme Wake duniani. Kwanza taifa la Waashuru lilitwaa mateka kabila za kaskazini mwa Israeli, kisha Wababli waliwachukua mateka kabila ya Yuda iliyo kuwa upande wa kusini.

Tunaweza kusali wakati wowote, kama mara nyingi tunapotaka, tuwapo nyumbani au safarini au kazini. Yesu alipenda kutoka nje pekee, mapema asubuhi, mahali fulani palipo kimya. Lakini pia tunaweza kuomba katikati ya dharura, kiasi kama tunavyoweza kumshukuru Mungu kwa mambo yanapokwenda vema na kwa baraka zetu zote, mara nyingi asubuhi au jioni. Bali kamwe tusidharau nafasi yoyote ua kusema na Mungu.

Maombi ya mwamini aliye batizwa

Mapema tumetaja katika somo hili kwamba kuna kitu maalum kuhusu maombi ya wale walio kwisha batizwa katika Kristo. Kiasi kama Kuhani Mkuu alivyokuwa ni mpatanishi kwa wana Israeli, hivyo Yesu Kristo ni mpatanishi kwa ajili ya wafuasi wake wa kweli.

Uhusiano huu maalum pamoja na Mungu katika Mwanawe ni kitu kingine cha kukitegemea kwa furaha, kama kwa neema yake Mungu, ukibitizwa.

Itamaanisha kwamba wakati ukikiri dhambi zako kwa Mungu kwa jina la Yesu Kristo atakusamehe dhambi zako - yaani atazifuta milele.

Yesu Kristo ni mpatanishi wa waamini waliobatizwa

Dhambi za watu wa Israeli hazikuondolewa wakati walipo toa sadaka za wanyama, kwa sababu wanyama hawana dhamiri ya kuhusu dhambi na hawawezi kutoa damu zao. Kama ilivyo andikwa kwa Waebrania 10:4: "Haiwezekani kwa damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi" Bali Yesu alikuwa ni sadaka kamilifu kwa sababu aliutoa uhai wake na maisha yasio na dhambi (Waebrania 9:12). Hivyo wale waliobatizwa katika Kristo wanae kuhani mkuu, alie pita katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu ...." ambaye alijaribiwa katika hafi zote kama sisi lakini hakutenda dhambi" (Waebrania 4:14, 15).

Yesu ni Kuhani Mkuu kwa waamini waliobatizwa

Ubatizo wa kweli wa Mkristo unamaana ya kuoshwa dhambi zetu (Matendo 22:16) na mara tukiisha batizwa tunaweza wakati huo kumkaribia Mungu kwa kupitia Yesu Kristo, katika ufahamu wa kweli kwamba "kama tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na haki kuweza kutusamehe dhambi zetu, na kututakasa na uchafu wetu wote" (1Yohana 1:9). Ndipo tutaweza kuitumia sala ya Bwana Yesu aliyowafundisha wafuasi wake:

> *"Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe. Ufalme wako uje. Mapenzi yako yafanyike, hapa duniani kama yanavyo fanyika mbinguni. Utupe siku kwa siku ridhiki yetu. Na utusamehe dhambi zetu; maana nasi pia tunawasamehe kila mmoja anaye tukosa. Na usitutie majaribuni; bali tuokoe nasi kutoka uovu" (Luka 14 :11:2-4).*

Hiyo itakuwa ni sala ya ajabu kuitoa; maana, "Heri aliyesamehewa dhambi, na kusitiriwa makosa" (Zaburi 32:1).

"Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako" (Zaburi 119:18)

Sisi sote tuombe ili kwamba Mungu abariki kusoma kwetu na kujifunza neno lake.

Je, Mungu atajibu?

Haja Yetu yoyote, tuilete kwa Mungu katika sala.

- Lakini siku zote atajibu?
- Je siku zote anajali?
- Siku zote anaweza kufanya yanayo hitajika?

Haya ni maswali yenye maana, na kuna majibu yaliyo wazi ya kutoka Biblia. Sala sio nafasi yetu ya kuweka kila kitu tunacho taka kwa Mungu, iii kwamba aweze kutoa kila kitu tunacho penda kuwa nacho. Sala ni sehemu ya ibada yetu, na inatupa fursa ya kutafakari mambo katikati mbele ya Mungu anaye tupenda na anayetaka kutupa kilicho bora. Mtume Paulo anasema:

"Msijisumbue kwa neno lolote" (maana yake, msiwe na wasiwasi) "bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu nazijulikane na Mungu" (Wafilipi 4:6).

Tuombe kwa imani, lakini tuombe kufuatana na mapenzi ya Mungu "Mapenzi yako yafanyike" Hii ina maana kusoma Biblia ili kutafuta mapenzi yake na makusudi, na sio kuomba vitu ambavyo tumeambiwa hatuwezi kupata. Wala tusisahau kwamba mara nyingi Mungu anajibu sala kwa kututaka tusubiri, wakati mwingine muda mrefu. Abrahamu aliomba, lakini ilibidi asubiri miaka mingi kupata mtoto aliye mwahidi Mungu. Wakati mwingine Mungu anajibu kwa kutokutupa tulicho omba; maana anajua kilicho bora, zaidi ya tunavyoweza kufanya, kile kilicho bora kwa ajili yetu.

Lakini kamwe haachi kutunza na kupenda. Siku zote, "Masikio yake yapowazi kuelekea kilio chao" (Zaburi 34:15)

Kujifunza kuomba

Twajifunza kuomba katika njia ili ile tunayo jifunza kusema - kwanza kwa kujifunza kutoka wengine, na kisha kujaribu kufanya kitukile kile sisi wenyewe. Basi inatubidi tuelekee kwenye Biblia kwa mfano. Biblia imejaa maombi, kama kitabu cha Zaburi ambapo kuna sala 150 zilizo tofauti za kuweza kujifunza, au maombi ya Yesu na wanafunzi wake.

Ikiwa tutasoma Maandiko kila siku akili itakuwa ya kumpendeza Mungu. Itatengeneza njia tunayo tumia kufikiri na kwa sababu hiyo namna ya kuongea na Mungu. Pia tunaweza kuwa vuta wengine kwa mwenendo wa kuwa mwanamaombi, kama kutoa shukrani kabla ya mlo pamoja na familia, au kupiga magoti pembeni mwa kitanda kabla ya kulala.

Watu walio gawanyika wakawa uhamishoni pasipo makao yao, na wakajikuta wenyewe wanaishi katika serikali zilizo abudu miungu mingine, sheria zao mara nyingi zilikuwa kinyume na zile za Mungu Mmoja wa Kweli.

Jinsi walivyo jiongoza katika hali (mazingira) hayo ni ya muhimu kwetu sana; maana wale ambao sasa wanakuwa watu wa Mungu wanaweza pia kuishi katika serikali zenye desturi na sheria ngumu.

Kumtii Mungu au binadamu?

Yaliyo wapata Danieli na rafiki zake yanatupatia mfano wa dhahiri wa namna ya kwenda katika mataifa tunayo ishi sasa. Walitwaliwa mateka na mfalme Nebukadneza wa Babeli alipo ivamia Yerusalemu na kuutwaa (yapata mwaka wa 600 KK), na tangu mwanzo wa kuhamishwa kwao walionyesha walikuwa wanaenda kumuweka Mungu kwanza katika maisha yao. Tazama mifano hii:

TATIZO	ALICHO FANYA DANIELI au RAFIKI ZAKE	MWISHOWE PALITOKEA NINI
Danieli na rafiki zake walipewa nyama iliyokuwa imetolewa kwa sanamu. Hawakula, lakini walijua hili jambo litamkasirisha mfalme na wakuu wake.	Hawakula nyama nao waka omba mboga za majani wapewe badala yake.	Mungu aliwatunza na waka onekana ni wenye afya kuliko wengine (Angalia Danieli 1:15-17.)
Nebukadneza aliwaambia watu wote wasujuda na waiabudu sanamu aliyo isimamisha	Refiki watatu Danieli walikataa kukiabudu kitu chochote kingine kuliko Mungu.	Walitupwa katika tanuru ya moto, lakini Mungu aliwao koa na hawakudhurika.
Maadui wa Danieli walitaka kumuondoa Danieli basi wali mshawishi mfalme mpya Dario akataze sala zote isipokuwa zilielekezwa kwake.	Danieli aliiendelea kama siku zote alivyo fanya na aliomba kwa Mungu huku madirisha ya chumba chake yakiwa wazi.	Alitupwa kwemye shimo la simba, lakini Mungu alimuokoa na hakudhurika.

Mifano hii inatufundisha sisi

- kumuweka Mungu awe wa kwanza katika maisha yetu;
- kushikamana na mambo yetu ya Mungu na si kupatana na pande mbili
- kwamba Mungu pekee ndiye aabudiwe.

Lakini Danieli na rafiki zake hawakuwa wafanya matatizo, kwa kutafuta nafasi ya kuvunja sheria za Mfalme na kupata sifa na kutukuzwa. Wakati sheria zile ziliopo patana sheria za Mungu, walikuwa ni watu washika sheria mno. Kweli kabisa wali kuwa ni miongoni mwa watumishi waliokuwa bora zaidi wa Mfalme na wakawa wakuu wa muhimu wa utawala, wakisimamia shughuli za mfalme.

Huu pia, ni mfano wa muhimu kwa wote ambao wanamfuata Bwana Yesu Kristo. Wakati sheria za Sherikali zinapo patana na sheria za Mungu (na sheria nyingi za wanadamu fikra zao ni namna moja au nyingine juu ya sheria za Mungu), basi yatupasa tuwe watu wanao fuata sheria pia. Kama Danieli, inabidi iwe kweli kwa sisi kuwa hakuna baya lolote pamoja na mwenendo wetu (ona Danieli 6:4,5).

Yawapasa Wakristo kutiisheria za Serikali (nchi wanazo ishi),
isipokuwa sheria hizi zikwa kuna tofauti na sheria za Mungu

Ufalme wa Mungu: katika siku za Yesu

Karibu miaka 2000, watu wa Mungu wameishi katikati ya mataifa ambayo yana sheria na mashauri yao wenyewe. Ilikuwa vilevile kwa Bwana Yesu mwenyewe: aliishi katika nchi ya Israeli kweny kipindi ambacho taifa lilikuwa chini ya utawala wa Warumi, na kwa sheria ile aliteseka na kufa. Lakini hakuwa mtu wa kufanya matatizo ya kisiasa, ingawa ndugu zake wengi - Wayahudi walitumainia angekuwa hivyo. Wala hakujaribu kubadilisha mamlaka ya Kiyahudi, ambayo ilikuwa inatumia vibaya nafasi zao katika hekalu na katika njia zingine.

Aliwahi kuulizwa mara moja kuhusu msimamo wake kwa mamlaka ya Kirumi, Yesu alionyesha jinsi sarafu ya Kirumi ilivyokuwa na sura ya kaisari (Mtawala wa Kirumi). Ndipo aliweka jambo la muhimu:

> *"Mpeni (yaani toeni) kwa njia hii mambo yaliyo ya Kaisari kwa Kaisari na kwa Mungu mambo yaliyo ya Mungu" (Mathayo 22:21).*

Hiyo inamaana kwamba tulipe kodi zetu, kama sheria inavyo taka (kitu kingine ambacho mtume Paulo anacho kilinganisha wazi katika Warumi 13:7, na kufanya kila kitu zaidi ambacho Serikali inatutaka kwa **muda ambao hakuna matata na matakwa ya sheria ya Mungu**. Tofauti hii ni ya muhimu sana, na ni moja ambayo Bwana Yesu kwanza alijizoeza mwenyewe siku zote alitoa kwa Mungu mambo yanayo husu Mungu, nasi tuwe hivyo.

Mamlaka wa Kiyahudi ilijaribu kumzuia Yesu kufundisha na kuponya. Lakini Yesu hakuacha hata wakati alipo wasunbua wazi na maisha yake kuwa hatarini, aliendelea tu na kazi yake ya wokuvu. Maana Yesu alijua kwamba kazi yake ilikuwa ni ya Mungu, na ndiyo aliifanya kuwa ya Kwanza. Hatimaye wakati alipo simama mbele ya Pontio Pilato na alipo kuwa katika nafasi ambayo angejaribu kujishughulisha na mamlaka ya Kirumi ili kuokoa maisha yake, Yesu alichuku nafasi hiyo kwa kuweka mambo kadhaa wazi. Kwanza, alimweleza Mtawala wa Kirumi kwamba ingawa yeye, Yesu, alikuwa ni Mfalme, Ufalme wake alikuwa bado kuja:

Tazama mifano iliyotolewa katika Zaburi 107:

- wenye njaa na kiu wamelishwa (mstari wa 5-6);
- wale wanao muasi Mungu, na kisha kutubu husamehewa (mstari 13);
- Mungu huwasikia wale ambao "wanakaribia kwenye milango ya. Mauti (mstari 18);
- Mungu huwasikia wale walio katika hatari ya kuharibikiwa na meli (mstari 28).

Fundisho limeelezwa kwa kifupi katika mstari 6:

> *"Ndipo wakamlilia Bwana katika dhiki zao, na akawaokoa kutoka katika shida zao"*

Tutawezaje kuongea na Mungu?

Katika Agano Jipya, wakati wa utumishi wa Yesu, Bwana ametuambia kuhusu mtoza ushuru ("watoza ushuru" na "wenye dhambi" wamedharauliwa na Wayahudi wengi) ambaye aliinamisha kichwa chake na kujipiga kifuani na aliomba "Mungu unirehemu mimi mwenye dhambi" (Luka 18:13) Yesu alisema mtu kama huyu atasikiwa na Mungu kwa sababu amenyenyekea mwenyewe (sio kama Mafarisayo, walio kuwa na majivuno mno ya kuishi maisha mema).

Kwa sababu hii tunaweza kuona kwamba Mungu siku zote anatoa njia kwa watu wanyoofu. Yeyote na mahali popote anapo ishi, ya kuweza kumkaribia kwa sala. Vilevile hata leo, tunaweza kujifunza masomo kutoka katika mifano mingi ya Biblia. Mwanaume au mwanamke anaye mtafuta Mungu na kusoma neno lake hakika ataona haja ya kuomba. Mungu hujishughu lisha na viumbe vyake na ataisikia sala yoyote iliyo nyooka.

Mtu amtafutaye Mungu atataka kumtolea utukufu na ibada ya kicho; kutoa shukrani kwa baraka zote za uzima na hasa kwa neno la Mungu, Biblia. Anapo jifunza kuhusu dhambi atapenda kuzikiri dhambi zake mwenyewe, na Mungu atamsikia.

(Lakini kuna kitu kimoja cha kujua: Mungu ata samehe dhambi kwa njia aliyo iweka, hiyo ni kwa sadaka ya Bwana Yesu Kristo, na hii inamtaka mwamini abatizwe kwanza.)
Askari wa Kirumi Kornelio alitoa mfano wa sala inayo kubalika. Tunasoma alikuwa ni -

> *"…mtu mtaua aliyemcha Mungu na nyumba yake yote, akiwapa watu sadaka nyingi sana, na alimwomba Mungu siku zote" (Matendo 10:1).*

Sala za Kornelio zilisikiwa na Mungu alimtuma mtume Petro ili kukamilisha mafunzo yake na kisha kumbatiza katika jina la Bwana. (Utasoma sura hii nzima mwisho wa somo).

Sala inayowezekana ya muhimu zaidi kwa mwanaume au mwanamke kujifunza kuhusu Mungu inapatikana katika Kitabu cha Zaburi:

Watu wa kawaida wanaweza kuzungumza na Mungu?

Kulikuwa hakuna njia nyingine ya kuja mbele za Mungu ila kwa kupitia kuhani wa Kiyahudi au kwa kutoa dhabihu?

Vipi kuhusu - watu walio ishi kabla ya kuwepo taifa la Israeli?
- watu waliokuwa sio Wayahudi?
- watu walio taka tu kuomba msaada kwa Mungu?
- wayahudi baadaye walio ishi katika nchi za kigeni?

Hawakuweza kuongea na Mungu moja kwa moja? Tunajua kutoka kusoma Biblia zetu na kuona mifano mingi ya sala iliyo tolewa kwa Mungu aliye mbinguni ambayo siku zote Mungu husikiliza maombi ya watu.

Kwa mfano, tunasoma: Mwanzo 24 kuhusu mtumishi wa Abrahamu, ambaye aliomba afanikiwe : kwenye safari yake ya kumpata mke mcha Mungu kwa ajili ya Isaka, mwana wa Abrahamu. Tunaweza kuona jinsi alivyo mshukuru Mungu wakati maombi yake yalipo jibiwa.

Tunaweza kusoma katika Ayubu 42 jinsi alivyo omba kwa ajili ya rafiki zake baada Mungu kumponya maradhi ya kutisha. Hanna, mama yake Samweli, alimwomba Mungu kwa sababu alikuwa hana mtoto. (1 Samweli 1 na 2), wakati Danieli akiwa utumwani Babeli, "madirisha ya chumba. chake yakiwa wazi kuelekea Yerusalemu alipiga magoti mara tatu kwa siku, na aliomba na kutoa. shukrani mbele za Mungu wake kama alivyo fanya tokea hapo" (Danieli 6:10).

Tena, tuna ombi la Mfalme Sulemani ili Mungu asikie sala ya wageni:

> *"Zaidi ya yote kuhusu mgeni naye, asiyekuwa mmoja wa watu wako Israeli atakapo kuja kutoka nchi iliyo bali sana kwa ajili ya jina lako; (maana watasikia habari za jina lako kuu, na mkono wako ulio hodari, na za mkono ulionyooshwa;) atakapo kuja na kuomba kuelekea nyumba. hii; basi usikie huko mbinguni, makao yako, ukatende kwa kadri ya ,yote atakayo kuomba mgeni huyo; ili watu wote wa dunia wapate kulijua jina lako, na kukucha wewe kama watu wako Israeli, nao wajue ya kuwa nyumba hii, niliyo ijenga, imeitwa kwa jina lako" (1 Wafalme 8: 41-43).*

Vipi kuhusu watu wote wale ambao wanamwita Mungu wakati wanapo kuwa katika shida? Atawasikia, hata kama wakati mwingine wamemsahau Mungu? Jibu ni ndiyo, ikiwa wanakuwa wanyoofu na wanyenyekevu na, wanao tubu.

> *"Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu: kama ufalme wangu ungekuwa ni wa ulimwengu huu, ndipo watumishi wangu wangepigana, ili waniokoe na mikono ya Wayahudi: bali sasa Ufalme wangu sio wa hapa" (Yohana 18:36)*

Dhahiri kabisa, Yesu alifundisha kuwa kutakuja kipindi cha Ufalme wake kuwekwa duniani (wakati atakapo tawala kwa uweza toka Yerusalemu), lakini kipindi kile wakati ale kilikuwa hakijaja, wala hata sasa bado. Bali, maana ya pili kwa Pilato ilikuwa kwamba Mungu hata wakati huo alikuwa ni mwenye kutawala; nyuma ya matukio Alikuwa anaongoza mambo, akisababisha mapenzi yake yafanyike. Maana kama Yesu alivyo mwambia Mtawala: "Usinge weza kuwa na nguvu kabisa juu yangu, usingepewa kutoka juu" (Yohana 19:11).

Mfano huo wa uaminifu wa Bwana Yesu ulifuatwa na mitume. Nao pia walikuwa waaminifu, raia wenye kushika sheria; kamwe hawakujiingiza katika mambo ya siasa, wao wenyewe walijitenga kutoka vyama vya taifa – kama kujiunga na jeshi la Kirumi, au kuangalia mashauri ya haki – bali walijitoa kwa utumishi wa Bwana. Lakini matata yalipokuja ama toka kwa Wayahudi au kwa Warumi na mamlaka zao, Mungu aliwekwa kwanza na kutii sheria sake. Kwa hivi, wakati mitume walipo ambiwa waache kuhubiri habari njema ya wokovu, jibu lao lilikuwa:

> *"Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:29*)

Ufalme wa Mungu: katika wakati uliopo

Mafundisho haya na mifano ni ya msaada mkubwa kwetu katika kuamua namna ya kujiongoza kame raia wa nchi ambazo zinatutaka sisi kufanya mambo magumu. Kama wafuasi wa Bwana Yesu, kuna mambo mengine tuyawake wazi, na shughuli zingine tuziepuke, ili kuzuia utata ambao pengine tunaweza kuwa nao kati ya sheria za Mungu na zile zilizo vumbuliwa na wanadamu.

Mungu awahesabu waamini wa kweli kama ni sehemu ya watu wake. Unapo soma 1 Petro2, utagundua kwamba lugha iliyo tumika kwanza na Mungu kwa Israeli (katika Kutoka 19) imekuja kuwa lugha ambayo wanaambiwa waamini wa Kikristo. Wamekuwa ni "kizazi kilicho chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu" (2:0), na ni kazi yao kuishi katika njia ambayo inamtukuza Mungu. Tambua kwamba wamekuwa ni taifa katika haki yao, ingawa kweli wametawanyika katikati ya mataifa tofauti – tofauti miongoni mwa ambayo wanaishi.

Kujitenga na ulimwengu

Waamini ambao sasa wanafanya sehamu ya taifa la Mungu, au Ufalme, wanamsubiri Mfalme wao kuja Yerusalemu. Atakapo kuja atawaita pamoja ili kutumikia, na kufanya kazi pamoja naye.

Inafuatia kwamba yawapasa wasifanye kitu chochote mpaka atakapo kuja ambapo atasimamisha uhusiano na Mungu: yapasa Mungu awe wa kwanza katika yote ambayo wanafanya. Hata hivyo, ingawa Mungu anafanya kazi nyuma ya matukio ili kuleta makusudi yake kukamilika, siku zote sio dhahiri namna itakavyo fanyika, wala watu geni na mataifa yapi ambao Mungu atayatumia.

Kinacho fuatia ni kwamba ni kosa kujiingiza katika utawala wa wanadamu, aidha katika sehemu maalum au taifa kisiasa, maana watu wa Mungu wanauhusu mpangilio wa mambo na tayari wana m falme, Bwana Yesu Kristo. Na vilevile ni kosa kujaribu kutumia taratibu za kisiasa za watu ili kuuleta ulimwengu katika hali nzuri – Mungu atafanya hivyo wakati Yesu ajapo. Kwa hiyo Mkristo wa kweli atakaa uje ya siasa, aidha kwa vitendo au kama mpiga kura.

Katika njia ile ile, ni muhimu kujiweka nje ya hali isiyo faa kwa mfuasi wa Kristo, kama kutengeneza silaha za kuteketeza au mabomu. Kuchukua kiapo, cha kutii Serikali au kwa mtawala wa duniani pia kuepukwe. Kama ilivyo elezwa mapema, Mkristo atakuwa mtii kwa sheria za Serikali (angalia, kwa mfano, 1 Petro 2:17) lakini ikiwa kuna nafasi ya kuchagua uaminifu wa mwanaume au mwanamke yapasa uwe kwa Kristo.

Kwa sababu hii haushauriwi kujiunga na Jeshi la aina yoyote, na wale ambao tayari ni wanajeshi wa aina yoyote kabla ya kuja kuielewa nuru watakuwa na haja ya kuombea kuhusu jambo hili na kutaka mwongozo kutoka kwa wafunzi wao wa Kozi. Mungu anao uwezo wa kukutafutia njia ya kutokea kutoka kwenye shida zote.

Itakuwa imeeleweka vema kwamba haja ya kujitenga kutoka kwenye siasa na kutoka kwenye kazi zilizo na shida hauonyeshi ubaya wa siasa na katika hoja namna ya matendo ya Serikali. Mambo haya yanatumika katika njia ileile iliyo sawa kwa waamini kila mahali. Kwa sasa, wapo chini ya “sheria ye Kristo” (1 Wakorintho 9:21) na yawapasa kuishi kwa kulingana za nazo. Kama mtume Paulo alipo sema, kuhusu kanuni zote na ulimwengu na matatizo:

> *“Tokeni kati yao, na mjitenge, asema Bwana, msiguse kitu kichafu; nami nitawapokea” (2 Wakorintho 6:17)*

Kujitenga kwetu toka kwenye njia na matendo ya desturi ma uongozi wa mwanadamu ni sehemu ya kuitwa kwetu kutoka katika ulimwengu, ili tuweze kweli kuwa wa Mungu.

Muhutasari

1) Yatupasa kutii sheria za Mungu.
2) Inatubidi kutii sheria za nchi yetu isipokuwa wakati hizi zikiwa na utata na sheria za Mungu.
3) Yatupasa kuepuka kazi yoyote, shughuli au kuzifuata ambazo zinaweza kutui ngiza katika matatizo kati ya sheria za Mungu na za wanadamu.

Mistari ya kusoma: Danieli sura ya 3 na 6; Warumi 13; Mathayo 22:15-22

Jifunze kwa moyo: 1 Petro 2:9-11

KOZI YA BIBLIA KUTOKA CHRISTADELPHIAN Na. 35

SALA

Kusoma: Zaburi 107

Kuweza kumuomba Mungu aliye mbinguni ni kitu cha ajabu. Ni tuzo ambayo amempa kila mmoja aliye mnyenyekevu na anayetambua kwamba Mungu ameumba kila kitu kilicho katika dunia. Sala inaweza kuonekana kuwa ni jambo gumu, kwa sababu kuna tofauti hii kubwa kati ya Muumba aliye mbinguni na viumbe vyake duniani. Hata sasa Mungu siku zote ameweka wazi kuwa anayo nia ya kumkaribia, na kwa wanaume na wanawake kusema naye ikiwa wana roho ya kweli na kama wapo tayari kulipokea neno Lake.

> *"Bwana asema hivi, Mbingu ni kiti changu cha enzi; na dunia ni mahali pa kuwekea miguu yangu..... bali mtu huyu ndiye nitakaye mtazama mtu aliye mnyonge aliye pondeka roho. Atetemekaye asikiapo **neno** langu" (Isaya 66:1,2).*

Kwa hiyo tuna ahadi kwamba Mungu atajibu kama tukija kwake katika unyenyekevu wa kweli. Tunaweza kufikiri kwamba sio rahisi kuongea na Mungu mojakwa moja. Kweli, katika nyakati za Agano La Kale watu mara nyingi waliogopa, sana walipo ona, kuwa wapo mbele ya Mwenyezi. Kwa mfano, watu Wa Israeli walipo toka Misri, utukufu wa Mungu ulishuka juu ya Mlima Sinai na kila mmoja, ukimjumuisha Musa aliogopa. Wakati Mungu alipo ongea nao watu walianguka nyuma na walisimama mbali (Soma Kutoka 9:17-20 na 20:18-21.) Mungu alikuwa anakaribia kwa taifa lake teule, lakini huu ulikuwa ni wangavu na uweza wake walijiona wasinge kuja mbele ya utakatifu Wake. Pengine nasi tungejiona vilevile. Waliogopa mno kiasi kwamba walimwomba Musa awe ni mpatanishi wao (au awe anaye simama kati) na Mungu. Basi hiyo ikawa ni njia ambayo Mungu aliwasiliana na Israeli - kwa kupitia zaidi mtu mwingine.

Hema ya kukutania ilipo jengwa kama mahali pa kufanyia sala jangwani utukufu wa Mungu uling'aa na juu ya "sanduku la agano" katika patakatifu pa patakatifu. Hakuna mtu alikwenda "mbele ya Mungu" isipo kuwa kuhani mkuu kila siku moja ya mwaka, kwenye siku ya kufanya upatanisho. Siku hiyo alikuwa ana omba msamaha mbele ya Mungu kwa dhambi za taifa la Israeli, na kwa vizazi vingi huu ulikuwa ni mfano mzuri kwa Wayahudi Walimkaribia Mungu kwa njia aliyopanga (Ilitabiri mambo ya mbele kwenye kazi ya Yesu Kristo akiwa mpatanishi kwa ajili ya Wafuasi wake. Alipokwenda mbinguni akawa "ni kuhani mkuu mwaminifu" kwa wale wanafunzi wote, iwe Wayahudi au la, walio batizwa "katika Kristo". Baadaye tutarudi kwenye somo hili.)